



*Mchungaji Tony Alamo
picha ya mwaka 1986*

Enyi mifupa mikavu, lisikieni neno la Bwana. Bwana MUNGU aiambia mifupa hii maneno haya; Tazama, nitatia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi. Nami nitatia mishipa juu yenu, nami nitaleta nyama iwe juu yenu, na kuwafunika ngozi, na kutia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi.³

Israeli, kama taifa, walijua kwamba wamekwisha.⁴ Hadi leo wamegawanyika pasipo matumaini. Lakini Mungu alimwambia Ezekieli kwamba ataliinua taifa lingine kubwa zaidi ya taifa la kwanza la Israeli, ambalo halikukoma kutenda dhambi. Taifa la pili la Israeli lingekuwa la watu kutoka kila taifa ulimwenguni,⁵ masalio ya Wayahudi wateule, kusanyiko kubwa la watu wa Mataifa waliopandikizwa kwenye Mzabibu wa Kweli (yaani, Kristo).⁶ Lingekuwa taifa kubwa, takatifu la wale waliofufuliwa kutoka kwenye maisha ya mauti ya dhambi hadi kwenye uzima wa milele.⁷ Hawatatenganishwa kamwe mbali na Mungu. Huu ndio uliokuwa



USHUHUDA WA TONY ALAMO

Mifupa Mikavu

na
Tony Alamo

Nabii wa Agano la Kale aitwaye Ezekieli, alipewa maono na Mungu. Aliona bonde la mifupa mikavu lililowakilisha hali ya kifo cha kiroho cha Israeli na dunia yote. Maono haya yalitabiri ujio wa kwanza wa Kristo, kuhubiri kwake injili, na matokeo yake; na ufuluo wa kwanza kutoka mautini kuelekea uzima wa milele kwa wote waaminio “Neno la Bwana.”¹

Mungu akamwambia Ezekieli, “Mwanadamu, je! Mifupa hii yaweza kuishi?” (Je, walikufa kiroho wanaweza kuishi?) Ezekieli akajibu, “Ee Bwana MUNGU [uliyewaumba], wajua wewe.”² Mungu akamwambia tena nabii, akasema, “Toa unabii juu ya mifupa hii, uiambie,

ufufuo wa kwanza kupitia kwa njia ya nguvu ya ufuluo ya Kristo.⁸

Katika mwaka wa 1964, kabla ya ufuluo wangu wa kwanza kupitia Kristo, mimi, Bernie Hoffman, pia ninayefahamika kama Tony Alamo, nilifahamika vizuri sana kwa utendaji dhambi na kwa mambo machafu, na sikuwa na ufahamu wowote kumhusu Mungu. Sikuwa na wazo kwamba Mungu yupo. Maneno ya Mungu kwangu yalikuwa kama hekaya na visasili, na sikuweza kuelewa jinsi watu wanavyoweza kumwamini Mungu au Mwana wake. Sikuweza kuwaamini wale amba walisema walimwamini Mungu kwa sababu walikuwa wanafiki. Walitenda dhambi kama mimi, au hata zaidi yangu. Najua hayo kwa sababu tulijuana kwa karibu. Sote tulikuwa kundi la mifupa mikavu iliyokufa. Ningepandwa na hasira kama ye yote angethubutu kunigeuza niingie kwenye Ukristo kwa sababu, kwangu mimi Biblia ilikuwa ni upotezaji wa muda tu. Maisha niliyoishi hayakunipa

muda wa michezo wala hadithi za kubuni.

Katika ulimwengu wa kibashara nilichukuliwa kuwa namba moja. Nilikuwa nikihusika katika ufanikishaji wa shughuli za waimbaji na waigizaji wengi wa kimataifa, na pia kutangaza kwa mafanikio bidhaa nyingi za matumizi ya nyumbani. Nilichoogopa kabisa wakati huo kilikuwa kwamba kama ningokoka ningesambaza kwenye kona mitaani vipeperushi vya injili inavyomhusu Yesu, ningeishi kwenye misheni duni na yenye kelele, ningehubiri injili na kupanga watu wenye njaa kwenye mistari ili wapate chakula.

Mnamo katikati ya miaka ya 60, dunia haikuonekana nzuri kwangu. Sikupenda madawa ya kulevyau watu wachafu waliokuwa na maadili ya nguruwe. Nilichukia sana kile ambacho vuguvugu la Hipi likiwa likifanya kwa Hollywood, Sunset Strip na dunia nzima. Kwangu mimi mwenyewe, (Inaendelea ukurasa wa 2)

1 Eze. 36:1, 4 **2** Eze. 37:3, asili yake ni Kiebrania **3** Eze. 37:4-5, asili yake ni Kiaramu **4** Eze. 37:11 **5** Mwa. 17:4-16; 22:18; 26:4; 46:3; 48:19; 49:10; Kut. 19:6; 32:10; Zab. 22:27; Isa. 2:2; Yoh. 11:51-52; Mdo. 10:34-35; Efe. 1:10; Ebr. 8:8-12; 1 Pet. 2:9-10; Ufu. 5:9; 14:6 na vifungu vingine vingi. **6** Yoh. 15:1; Rum. 11:17; 19, 23, 24; Ufu. 7:4 **7** 1 Pet. 2:9 **8** Rum. 15:12; 1 Kor. 15:15, 16; Kol. 2:12; 3:1; 1 Thes. 4:16; Ufu. 20:5-6

USHUHUDA WA TONY ALAMO

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)

sikuwa mtakatifu. Sikujali kile watu walichokuwa wakikifanya hasa katika kutenda dhambi, ila tu wasikifanye hadharani kwa lengo la ushawishi mbele ya familia yenyewe watoto. Kwangu mimi, dunia ilikuwa imekwisha, imekufa, imekauka, ya kuchukiza na isiyo na matumaini.⁹ Hakukuwa na kitu kilichokuwa na thamani yoyote tena. Naamini watu wengine hapa dunia waliyafahamu haya kama mimi nilivyoyafahamu, na ndiyo sababu walitumia madawa ya kulevya ili waweze kuepuka uhalisia wa hayo. Makanisa yalikuwa manafiki; kila mmoja alionekana kufahamu hilo pia. Dunia nzima ilikuwa imekufa katika dhambi na makosa yake.¹⁰ Dunia ilikuwa bonde kubwa la mifupa mikavu, sawasawa na lile aliloliona Ezekieli.¹¹

Nilikutana na Yesu nikiwa katika ofisi ya Beverly Hills kwa njia isiyokuwa ya kawaada. Hakuna mtu anayeweza kufikiria namna nilivyokuwa na hofu na bado nikawa na furaha pia wakati Mungu aliponithibitishia kuwa yeye na Mwana wake wapo na wanaishi. Nili-sisimka kukutana na Roho Mtakatifu wake wa ajabu na kuisikia sauti yake yenyewe nguvu ikipita kila sehemu ya kiungo cha mwili wangu kana kwamba nilikuwa kichujo; ambapo maneno yake yalikuwa yakienda mbele na kurudi nyuma. Uwepo wake ulijawa na utukufu na joto. Roho wake alinigandamiza kwa nguvu sana kama vile nilikamatwa kwa nguvu na mkono wa Mungu. Kisha akaniambia maneno haya, "Simama kwa miguu yako mwenyewe na uwaambie watu walio kwenye chumba

hiki habari ya Bwana Yesu Kristo, na kwamba anarudi tena ulimwenguni, usipofanya hivyo kwa hakika utakufa." Wakati Roho wake alipokuja ofisini na kunigandamiza, nilipewa ufahamu wa hekima yake ya ajabu isiyoweza kuelezeza.¹² Alikuwa kila chembechembe na molekuli kwangu. Alikuwa [kama] hewa. Alijuwa kila kitu cha siku zilizopita na kila kitu ambacho kingetokea katika siku zijazo.¹³ Niliteseka kwa kuwa nilijua kwamba alifayahamu yote niliyokuwa nimeyatenda. Kisha akanionesha kwamba, Mbingu na Jehanamu kwa hakika zipo. Katika sehemu hizi mbili nilifahamu ni ipi niliyokuwa nikielekea kama sitafanya alichoniambia...na hai-kuwa Mbinguni.

Ingawa lilikuwa jambo la kuniogofya,¹⁴ pia lilikuwa jambo la ajabu na la kustaajabisha kujua kwamba, kwa hakika Mungu yupo na anaishi na kila kitu walichosema manabii na mitume kumhusu yeye ni kweli. Hajabadilika kamwe tangu siku alipoumba mbingu, dunia na vyote viliyvomo.¹⁵ Kwa haraka nilijua kwamba, daima nitamhofia, nitamhusudu, nitamheshimu, nitampenda na kumtumikia. Nilijua kwamba nitakuwa tayari zaidi ya kuishi, kuteswa na kufa kwa ajili yake na kufanya hivyo kwa uchangamfu na furaha yote.¹⁶

Baada ya Mungu kuniondoa kutoka kwenye ofisi ile, nilianza kumwuliza, "Unataka nifanye nini? Nitafanya chohote utakachosema." Sikupata jibu, hivyo nikaanza kufikiria kuwa alitaka niende kanisani. Nilifikiria kanisa kubwa ndilo bora; hivyo nikaenda huko, lakini sikumpata huko. Basi nikaenda kwenye makanisa mengine, lakini hata huko pia sikumpata. Kisha nikasoma vitabu ambavyo majalada yake yali-kuwa na picha za watu walioonekana wenye hekima na wamchao Mungu, wenye ndevu ndefu na mavazi ya kidini, lakini nilijua vitabu hivi vilikuwa

na kasoro kwa maana vilisema kuwa Mungu si wa kuogopwa,¹⁷ kwamba Mungu hawatishi watu, na kwamba unaweza kutenda dhambi na usiende Jehanamu.¹⁸ Sikumwogopa Mungu wa aina hiyo; nilimwogopa Mungu aogo-fyaye,¹⁹ Mungu aliyenionesha Mbingu na Jehanamu; akanifanya nitende kitu ambacho hakuna mwanadamu ye yote ambaye angenifanya nikitende, kitu ambacho sikutaka kikitenda.

Sikuwahi kufikiria kwamba ukweli ungeweza kupatikana kwenye Biblia, kwani zilikuwepo kweli nyingi na zilipatikana kila mahali. Nilihiis kwamba kitu ambacho watu wengi walivutiwa nacho hakikuwa kizuri, kwani niliamini kuwa watu wote walikuwa wapumbavu. Hati-maye nilianza kusoma Biblia, na humo ndani niligundua mpango wa wokovu na maelekezo ya uzima wa milele am-bayo yalieleza namna ya kukua katika Kristo na kukua kiroho ili niwe chombo kikuu cha kuleta watu kwa Yesu.²⁰

Wakati nilipoanza kusoma Biblia, nilihisi kuwa nguvu zile zile za Mungu zilikuwa zikinigandamiza, ambazo nilizihisi nilipokuwa kwenye ofisi huko Beverly Hills. Kisha Mungu akanionesha maono mengine ya Mbinguni na Je-hanamu.²¹ Nikamlilia Mungu, "Bwana, usinipeleke Jehanamu!" Kisha nikapona Mbinguni na kujisikia amani ya Mbinguni.²² Ingawa nilikuwa kipofu, uchi na mchanga kiroho, nilimwambia Mungu kuwa ningependa kubakia kip-ofu, uchi na nisiye na umuhimu wowote kama daima nitaendelea kuisikia amani hii ya mbinguni. Kwa mara nyingine tena nikaiona Jehanamu na nikamlilia Mungu anirehemu na kunisamehe. Kisha nguvu za Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ziliingia mwilini mwangu.²³ Kwa imani yangu katika Yesu na damu aliyotoa kwa ajili yangu, na kwa imani yangu katika Neno la Mungu nililosikia na kulitii;²⁴ nilijisikia kila dhambi

⁹ Mat. 13:39, sura 24; 1 Kor. 15:24; Ebr. 9:26; 1 Petro 4:7

¹⁰ Efe. 2:1, 5; Kol. 2:13 ¹¹ Eze. 37:1



¹² Hes. 24:16; 1 Sam. 2:3; Ayu. 21:22; Zab. 32:8; Mit. 2:6; 3:20; 9:10; Lk. 1:77; Rum. 11:33; 1 Kor. 1:25; 2:16; 3:19; 2 Kor. 4:6 ¹³ Zab. 44:21; 94:11; Isa. 46:9-10; 1 Kor. 3:20; 1 Yoh. 3:20; Ufu. 21:6, 22:13 ¹⁴ Mwa. 35:5; Law. 26:16; Ayu. 31:23; Yer. 32:21; Eze. 32:32; 2 Kor. 5:11 ¹⁵ Mwa. 1:1; Mal. 3:6; Mdo. 4:24; 2 Kor. 5:11; Ebr. 13:8 ¹⁶ Zab. 5:11; 35:19; Isa. 51:11; 61:10; Yoh. 16:33; Mdo. 2:28; 20:24; Rum. 12:8; 15:13; 2 Kor. 8:12 ¹⁷ Mwa. 22:12; Zab. 11:2; Mit. 13:13; 14:16; 28:14; 31:30; Mhu. 7:18 ¹⁸ Mit. 8:36; Eze. 18:2, 4; Ufu. 19:20; 20:10, 14, 15, 21:8 ¹⁹ Mwa. 2:17; 6:7, 9, 13; Kut. 20:5; 32:33; 34:7; Eze. 3:18; 18:20; Mat. 8:12; 22:13; Mk. 16:16; Ufu. 2:5, 16, 22-23; 3:3; 20:15 ²⁰ Yoh. 4:35-36; 15:5, 8, 15-16; Ufu. 14:18 ²¹ Isa. 5:14; 14:9; Lk. 16:22-31; Mdo. 7:55-56; Ufu. 4:1-11; 14:10-11; 15:1-4; 20:10; 21:2-5, 10-27; 22:1-5 ²² Rum. 5:1; Efe. 2:14; Flp. 4:7; Kol. 3:15; 1 Thes. 5:23; 2 Thes. 3:16 ²³ Law. 26:11-12; Yoh. 14:16; 2 Kor. 6:16; 1 Pet. 2:5; 1 Yoh. 3:24 ²⁴ Hab. 2:4; Mat. 17:20; Lk. 7:50; Mdo. 20:21; 26:18; Rum. 1:17; 3:28; 5:2; 10:17; 11:20; Gal. 2:16; 3:11; Efe. 2:8; 3:17; Ebr. 10:38

niliyokuwa nimeitenda ikiondolewa rohoni mwangu.²⁵ Nilijisikia msafi na niliyetakasika.²⁶ Kitu cha ajabu sana kilikuwa kimenitokea, na kilifanywa kwangu na kwa ajili yangu na Kristo Yesu, "Mtakatifu wa Israeli."²⁷ Nilikuwa mwenye furaha sana kuwa huru kutoka dhambini na kumiliki nguvu hizi mpya ambazo zilinifanya nisitende dhambi ambazo nilitaka kuiambia dunia yote ili nao waweze kumjua yeye na kupata uzima wa milele.

Hata baada ya kuwa kwenye huduma ya Kristo tangu mwaka 1964, kila nisomapo Biblia ninahisi afya ya kiroho ikitiririka kutoka mbinguni na kuingia kwenye mifupa hii ambayo wakati mmoja ilikuwa mikavu. Neno la Mungu limeweka mishipa ya kutia nguvu ya kiroho kwenye mifupa hii ambayo wakati mmoja ilikuwa mikavu, na kuiwekea nyama na ngozi ambayo ni silaha ya kiroho. Kila Neno la Mungu limempandikiza Yesu zaidi moyoni mwangu. Bado ninaweza kuhisi kila Neno la Mungu likipumua pumzi ya Roho Mtakatifu nafsi mwangu, likinipatia nguvu za kusimama na kuzima mishale yote ya Shetani aliyonirushia

(Inaendelea ukurasa wa 8)

25 Mk. 14:24; Yoh. 6:53; Mdo. 20:28; Rum. 3:25; 5:9; Efe. 1:7; 2:13; Kol. 1:14, 20; Ebr. 9:12, 14, 22; 1 Pet. 1:18-19; Ufu. 1:5, 5:9 **26** Ebr. 10:19-22; 1 Yoh. 1:7; Ufu. 1:5; 7:14 **27** Zab. 89:18; Mdo. 3:13-14

Tanzania

Kwa Mchungaji Alamo, mpendwa wangu na Mchungaji tuliyepewa na Mungu,

Neema, rehema na amani kutoka kwa Baba na Bwana wetu Yesu Kristo iwe juu yenu na juu ya huduma yenu. Ninamshukuru Mungu, am-baye nimemtumikia tangu mwaka 1994. Mimi ni mwinjilisti kutoka Musoma, Tanzania. Nimekuwa nikijitahidi kupanua huduma yangu ili ifike nchi nzima na hata nje ya nchi ya Tanzania. Hivyo Mchungaji, japo sijapata kusikia sauti yako wala mahubiri yako au hata kuona uso wako; kwa kupitia makala zako ambazo huwa nazipokea na kusoma habari za kustaaabisha, kama vile "Mifupa Mikavu", "Masih" na "Shamba la Mungu"; nimeelewa haja yako ya sasa na ya baadaye kuhusu kanisa ambalo ni mwili wa Yesu.

Mimi na wahudumu wenzangu katika Bwana, na pia waumi-ni wapya ambao wamemkubali Yesu kupitia makala zako, tumeanzisha ushirika unaoitwa Believer Community Church

(B.C.C.). Tungependa kupanua huduma yenu katika Afrika Mashariki, hasa Tanzania, na hata kufika vijijini. Tafadhali Mchungaji, tunahitaji msaada wako. Kama utatutumia vipasa sauti, genereta, Biblia za kuwapa waumini wapya na makala za kufundishia; itatusaidia kufikia mahitaji yetu katika huduma hii ya injili na uinjilisti katika vitongoji. Kupitia haya Mungu atakubariki sana. Mungu aibariki huduma yako na kuyainua maisha yako ya kiroho kwa kazi njema ambayo unaifanya. Tunashukuru na tunasubiri kwa dhati majibu yenu mazuri. Wako katika Yesu,

O.E.M. Tanzania, Afrika Mashariki

Kalifonia

Mpendwa Mchungaji Alamo,

Ninaandika waraka huu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na nikiwa kamili kivita, yaani nimevaa silaha zote za Mungu (Wafe-feso 6:10-17). Hivi majuzi, kwa kupitia hali ya kukua kiroho na kwa kupitia ushirika na ndugu yangu katika jeshi la Mungu, ukweli fulani na siri za Biblia zimefunuliwa kwetu kupitia Roho Mtakatifu. Ninajua kwamba Mungu anawaandaa wateule wake sasa, na nilifahamu hivyo baada ya kupitia ukurasa mmoja katika mojawapo ya machapisho yako. Sina budi kusema kwamba Mungu ameleta makala hizi kwangu katika wakati mwafaka ninapohitaji kujua kweli fulani. Zaidi, nimefurahishwa sana na huduma yako. Wewe unasema ukweli mbichi bila kuupaka sukari na kunifahamisha utamu wote wa unabii. Tafadhali, nihesabu kuwa mmoja kati ya wanachama wako na kuni-weka kwenye orodha ya wanaotumiwa makala hizi; ili niweze kukua katika Roho Mtakatifu, nikijiamini kwa Neno la Mungu la kweli. Niko kwenye gereza la jimbo, na huku haturuhusiwi kuwa na vitabu vilivyo na ngozi ngumu. Sina uwezo wa kuwasaidia kifedha, lakini maombi yangu kwa huduma yenu yenyeye nguvu ni kufanikiwa kwenye kazi yako yote.

Wako Mwaminifu,

B.L.

Corcoran, Kalifonia



Mhudumu wa Tony Alamo Christian Ministries, mchungaji M.C. akisambaza vijarida vya Mchungaji Alamo — Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Kwa ndugu mpendwa na kiongozi aliyethaminiwa kiroho, kasisi Tony Alamo,

Pokea salamu nyingi kutoka kwa ndugu zenu hapa India na kwenye Huduma ya Kikristo ya Tony Alamo ya India. Nilifurahi sana nilipopokea Biblia na machapisho mengine yakijumuisha "Masihi". Kwa maombi, mimi pamoja na ndugu zangu Wakristo tunasambaza mpango wa kweli wa ukombozi kwa wale wanaojua Kiingereza na tunajaribu kutafsiri makala hizi za ajabu kwa lughamama yetu kwa wale ambao hawajui Kiingereza na wanaokaa vijijini. Watu wengi wakiwemo madereva, wanafunzi wa shule za upili [sekondari], vyuo vyaa udaktari na uhandisi, wafanyakazi katika viwanda, waalimu na wote walipokea makala hizi; wanazidi kubarikiwa na makala hizi zinazobeba mpango wa ukombozi wa kweli. Watu wengi wamem-pokea Yesu katika maisha yao katika jiji letu. Tunaomba uikumbuke huduma yetu katika maombi yako yenye thamani.



Ndugu T.R. akisambaza kitabu ambacho kimegusa roho za watu wengi cha mchungaji Alamo, The Messiah [yaani "Masihi"] — Rajahmundry, India

Kwa heshima, ndimi mtumishi wako katika shamba la Mungu.

Wako Mwaminifu,
Mchungaji N.T.
Rampachodavaram Mandal
India

Yehova aliweka "juu yake Maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:6). Masihi alikuwa mkombozi mwenye asili ya Mungu, ambaye alikabiliana na miale mikali ya moto wa hukumu ambayo ilimpasa mwanadamu. Je, neema ya Mungu ni ya ajabu namna gani kupitia dhabihu ya Yesu kwa niaba yetu! Hivyo, kwa mara moja msalaba ukawa fedheha kuu kwa Kristo, lakini pia ukawa utukufu wake mkuu – na njia ya pekee iliyochaguliwa ya kuwalettea wokovu wanadamu.

Wakati Bwana Yesu alipokuja, alimiza unabii wote huu kupitia kifo chake cha upatanisho pale msalabani "Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti" (1 Petro 2:24).

(10) **Masihi ATAJITOLEA kuteseka na tena bila kulalamika, Isaya 53:7:**

"Alionewa, lakini alinyenyekeea, Wala hakufunua kinywa chake; Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, Na kama vile kondoo anyamazavyo Mbele yao wakataa manyoya yake; Naam, hakufunua kinywa chake."

Watu wengine wanaoteseka hunung'unika na kulalamika, hasa wanapodhulumiwa – lakini haikuwa hivyo kwa Masihi. Alijitoa mwenyewe kwa jukumu aliloteuliwa la "kubeba

Hii ni dondoor kutoka kwenye kitabu cha Mchungaji Alamo, The Messiah

Mwujiza Mkuu Unaochapishwa:

**Historia ya
Masihi**

Kwa mujibu wa Unabii wa Biblia

"Huyo manabii wote humshuhudia" (Matendo ya Mitume 10:43).

"Katika gombo la chuo nimeandikiwa"

(Zaburi 40:7; Waebrania 10:7).

**(B) Inaendelezwa kutoka Isaya 53.
(9) MATESO ya Masihi KWA NIA-
BA YETU, Isaya 53:4-6, 8, 10-12:**

**"Hakika ameyachukua masikitiko
YETU, Amejitwika huzuni ZETU; ...
Bali alijeruhiwa kwa makosa YETU,
Alichubuliwa kwa maovu YETU;
Adhabu ya amani YETU ilikuwa juu
YAKE, Na kwa kupigwa KWAKE SISI
tumepona... Na Bwana ameweka juu
YAKE Maovu yetu sisi sote... Alipig-
wa kwa sababu ya makosa ya WATU
WANGU... Utakapofanya nafsi yake
kuwa dhabihu kwa dhambi... Naye**

**atayachukua maovu YAO..." "Walaki-
ni alichukua dhambi za watu wengi."**¹

**Kinachodhahirika wazi katika sura
hii ni ile hali ya kuteseka ya Masihi
kwa niaba, [au] kwa ajili ya wengine.** Sura hii ina vifungu kumi na viwiliwili tu; lakini kwa mara kumi na nne imetaja fundisho la sadaka kwa niaba ya dhambi ya wanadamu wote. Sehemu yote (Isaya 52:13-53:12) imefurika dhana hii, na siri hii haikupatiwa ufumbuzi hadi Yesu alipofanywa kuwa "dhambi kwa ajili yetu" (2 Wakorintho 5:21) na "alikufa kwa ajili ya dhambi zetu" (1 Wakorintho 15:3).

¹ Mwandishi anayetumiwa na Mungu anazuia uwerekano wa uharibifu au masomo danganyifu yanayopinga mafundisho ya kuteswa kwa niaba ya mwingine kutoka kwenye kifungu hiki kwa kuyawasilisha mara nyingi, na kwa namna tofauti ambayo haibadilishi, kiasi kwamba anayefanikiwa sehemu moja analazimika kukutana nayo sehemu nyingine.

Kutoka kwenye laini yetu ya simu ya maombi na habari iliyo wazi saa ishirini na nne:



Mchungaji Mike Omoasegun pamoja na baadhi ya washiriki wake hupata makala mbalimbali za Mchungaji Alamo na Biblia za King James Version kutoka katika Huduma ya Kikristo ya Tony Alamo — Suleja, Nigeria

dhambi zetu” na kujipeleka kama mwanakondoo machinjioni. Kwa kimya kikuu kilichojawaa na msamaha, Masihi atavumilia mateso makuu mpaka mwisho, kwani Yehova anataka hayo. Na hapa tunatazama kwa kina siri isiyoelezeka ya upendo usio na mpaka.

Katika Agano Jipya, Yesu Kristo alipigwa, alinenewa uongo, alitendewa vibaya, alitukanwa, alitemewa mate, aliteswa, alisukumwa huku na huko, alichapwa mijeledi na alisulubiwa; hakuwa na hasira yoyote wala chuki kwa waliomsulubisha, hakutoa kwa sauti malalamiko yoyote, bali maombi.

Baada ya mashahidi wengi wa uongo kumnenea uongo, kuhani mkuu alimwuliza, “Hujibu lolote?... lakini Yesu akanyamaza” (Mathayo 26:59-63).

Haya ni maombi ya Yesu akiwa anateswa na kusulubishwa msalabani: “Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo” (Luka 23:34).

Utaratibu huu wote ulikuwa si wa kawaida, ni kinyume na asili na hali ya kibinadamu. Mtu hawesi kuvumilia ila

kushtuka na kushangazwa na unabii huu wa ajabu; na zaidi ya hayo yote kushangazwa na utimilifu wake wa ajabu.

(11) Atakapotolewa gerezani na hukumuni, Masihi HATAKUWA na WAKILI wa kumtetea, hatakuwa na rafiki atakayesema kuwa hana hatia, Isaya 53:8:

“Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; Na maisha yake ni nani atakayeisimulia?”

Baraza la Israeli ambalo lilijumisha wakuu wa makuhani, wazee na waandishi lilikuwa na mazoea kuwaita wale waliojua kitu chochote cha kumtetea mshtakiwa kuja mbele yao na kukisema kwenye “kesi inayohusu mai-sha” ya mtu. Hili halikufuatwa wakati wa kesi ya Yesu wa Nazareti, bali kesi hiyo ilifanywa kwa haraka na ilikuwa jambo la kufedhehesha kwa baraza la Israeli; kwani baraza lilikuwa kinyume na kanuni zake lenyewe na dhidi ya viwango vyote vya haki na usawa. Hivyo mashtaka haya yaliharakishwa na kuen-

deshwa kinyume na kanuni na taratibu zao wenyewe na kinyume na viwango vinavyostahili vya haki.

Yesu alitakiwa kufika peke yake bila mtetezi mbele ya uongozi wa kifisadi wa Kiyahudi na mbele ya wawakilishi wa watu wa mataifa waliokuwa na nguvu wakati huo. **Hakuna hata mtu mmoja aliyejika kuchukua nafasi yake.** Yuda alikuwa amemsaliti; Petro alikuwa amemkana na wanafunzi wengine “wakamwacha, wakakimbia...” (Mathayo 26:56). Na wengi wa wanawake ambaao, wakati wa huduma yake walikuwa wakimhudumia, walismama “wakitazama kwa mbali” wakati alipokuwa akisulubishwa (Mathayo 27:55). Katika wakati alipokuwa katika uhitaji mkuu kibinadamu, **HAKUNA HATA MMOJA ALIYESIMAMA NAYE.** Kweli, baadaye, baada ya saa nydingi, uchovu na mwili ulioganda kutokana na mateso, Mariamu mama yake Yesu, wanawake waaminifu wachache, na Yohana mwanafunzi wake mpendwa, “walismama

(Inaendelea ukurasa wa 6)

Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni:—(661) 252- 4362

MASIHİ

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 5)

karibu” msalabani; lakini wakati wa mateso yake na wakati wa kusulubiwa kwake, alikuwa peke yake. Hakuna katika historia ya ulimwengu mtu ambaye amewahi kutelekezwa kabisa na rafiki zake pamoja na wapendwa wake kama alivyofanyiwa Yesu.

Yesu alikamatwa, SIO na maofisa husika, bali na genge la wafanya vurugu “kundi kubwa wenyepanga na marungu, wametoka kwa wakuu wa makuhani na wazee wa watu” (Mathayo 26:47). Hata Yesu aliongea kuhusu ukiukaji wao wa sheria zao wenye: “Je, mmetoka kama kumkamata mnyang’anyi, wenyepanga na marungu, ili kunishika? Kila siku naliketi hekaluni nikifundisha, msinikamate. Lakini haya yote yamekuwa, ili maandiko ya manabii yatimizwe” (Mathayo 26:55-56).

Mashahidi wa uongo walipewa rushwa ili kutoa ushahidi wa uongo dhidi ya Yesu ili “wapate kumwua” (Mathayo 26:59), na alihukumiwa (kesi yake ilifanywa) usiku, jambo lililokuwa ni kinyume na sheria.

Katika mahakama ya Kirumi, wakati Pilato alipokuwa akijaribu kupitia [mfumo wa] haki ili kumpata na hatia, aliwaliza watu, “Ni ubaya gani alioutenda?” Jibu pekee alilolipata kutoka kwa umati wa watu wakiongozwa na viongozi wao lilikuwa kelele zilizochewa na viongozi wao, “Na Asulubiwe ...na Asulubiwe” (Mathayo 27:22-23). Basi, Pilato alipotambua kwamba sababu iliyotolewa na haki havikufanya kazi na kwamba “ghasia” zaidi ilikuwa inaanza, akanawa mikono kwa shingo upande kuhusu suala hili kisha akamtoa Yesu kwao, ili wapate kumsulubisha (Mathayo 27:22-26). Hii ilikuwa njia mbaya zaidi ya kutekeleza haki katika kumbukumbu za historia yote.

Yesu hakupatikana na kosa alipojariwi na Pilato “mimi sioni hatia kwake” (Yohana 19:6)—na pia nabii wa kale aliyetoa unabii wa Masihi alisema, “Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake” (Isaya 53:9).

Itaendelea kwenye jarida jingine

Zambia

Mpendwa Mchungaji Tony Alamo,

Nina furaha tele kukuandikia waraka huu. Unaendeleaje Mchungaji? Naamini kwa neema ya Mungu Mwenyezi u mzima. Nilisoma kijarida chako kitiwachwo World Newsletter, “Viongozi na Waongo”. Mungu aliniwezesha kukipata kijarida hiki kimiujiza. Baada ya kukisoma, nilibarikiwa sana na nikaazimia kukuandikia waraka huu. Asante kwa ujumbe wa ajabu unaowafikia walipotea na wale ambao hawajaokolewa ili Kristo aumbike katika maisha yao. Kupitia makala yako, watu wengi wamefikiwa na kuokolewa kutoka kwa Ibilisi. Mungu akubariki kifedha, kimwili na kiroho.

Mchungaji, mimi na bado ni mwanamke kijana niliyeolewa miaka mitano iliyopita. Nilitoa maisha yangu kwa Yesu Kristo miaka miwili iliyopita na Mungu amekuwa mweema kwangu. Nina ndoto ya kuhubiri injili ya kweli kwa wengine. Kama wanawake wa Kiafrika tulivyo, tumekuwa tukifungwa na minyororo kwa karne nyingi kwa sababu ya tamaduni na kwa hivyo ninatamani sana kujitoa kwa Mungu. Mchungaji, ninaomba Biblia, vitabu, majarida, tepu zenye jumbe za Mungu na machapisho mengine ili kuniwezesha kuzifikia roho zilizopotea.

Hatimaye, ninaomba kusaidiwa na nyenzo za kuchambua Biblia na tepu za nyimbo.

Wako katika Kristo,
L.M.

Isoka, Zambia

Mpendwa Mchungaji Tony Alamo,

Pokea salamu zangu za dhati na furaha katika jina la Bwana Yesu Kristo. Ninamshukuru Mungu kwa maisha yako na jinsi alivyopanga kukutumia kwa namna bora kabisa kueneza injili ili ifikie pembe zote za ulimwengu kwa lengo la kuokoa maisha. Mheshimiwa Mchungaji Alamo, hapo awali kabla sijaokolewa kutoka maovuni na Yesu kwa msaada wa mfanyakazi mwenzangu, nilikuwa mpagani. Na wakati niliposoma kijarida chako, ujumbe niliousoma uliuweka moyo wangu mahali pazuri na pa hakika. Mungu anabadilisha maisha yangu. Kwa haraka nimeelewa kuwa Mungu anataka tujazwe na uadilifu. Mchungaji Alamo, ninaomba Biblia moja au mbili, moja yangu na nyingine ya rafiki yangu ili tuweze kulisoma Neno la Mungu. Basi, amani ya Bwana wetu iwe nawe na roho yako. Ninakushukuru kwa watu walio na mawazo mema, wanaojibu maombi yetu.

Asante,
G.N.

Kitwe, Zambia

Mexico

Aliyethaminiwa Mchungaji Alamo,

Makala yako imefika hata huku niliko na ina jumbe za kupendeza mno na shuhuda kutoka pande mbalimbali za dunia. Bila shaka, Mungu anakutumia kwa nguvu ili kuleta ujumbe wa ukombozi kwa kila binadamu. Nimekuwa gerezani kwa miaka saba na nusu kwa kosa la kusafirisha bangi. Kwa miaka miwili iliyopita, nikiwa hapa gerezani, Mungu alijidhihirisha kwa njia ya miujiza katika maisha yangu yaliyojaa dhiki. Ninatarajia kuachiliwa mwaka huu, na ningependa kujua iwapo utanitumia kitabu chako kitiwachwo *The Messiah [Masihi]* na makala nyingine ambazo zitasaidia kubadilisha watoto wangu.

M.A.

Monclova, Coahuila, Mexico

Barua kwa Mchungaji Alamo

Ghana

Mpendwa na Mchungaji mwema,

Nilijawa na furaha uliponitumia vijarida vyako. Nilipata kifurushi cha vijarida hivyo wiki iliyopita. Mpendwa mtumishi wa Mungu, watu walifurahi sana kuvisoma. Rafiki zetu wa vijijini ambao huwa tunawagawia zawadi na ambao huwa tunawatembelea kwa njia ya mikutano ya maombi, walikuwa na hamu ya kuvisoma na wengine wameguswa kwa kusoma barua kutoka kwa wengine. Tuna furaha na shukrani nyingi na tunaomba kuwekwa kwenye orodha ya watu wanaopokea makala nyingine za Injili. Tunahitaji Biblia, machapisho yako na tutafurahi tukipata mafundisho kutoka katika huduma yako.

Tunakuombea wewe, mwanao mpenda na Sion, na wote unaofanya kazi pamoja

Nigeria

Mpendwa Mchungaji,

Pokea salamu zangu kwa jina la Yesu Kristo, Amina! Vjarida vya mwisho ulivyonitumia, vyote vimesambazwa na ninashangazwa na mababiliko yaliyojitokeza katika maisha ya watu baada ya kuvisoma. Wame-toa ahadi kumtumikia Mungu kwa miyo yao yote na wengine wameahidi kukuandikia barua. Ningependa kuomba nakala 25 za kitabu kiitwacho *Masihi*, na vjarida vingine mbalimbali vipatavyo 150, Biblia chache, na makala nyingine ambazo zitatusaidia katika uinjilisti, kuwagawia rafiki, familia na watu wengine ambao wana nia ya kumjua Bwana Yesu Kristo. Ninataka sana kuwa mmoja wa wahudumu wako hapa Nigeria. Ningetaka kujua kinachohitajika. Nimeona kuwa mkoно wa Mungu uko juu yako na juu ya huduma yako na ningetaka pia kuchota neema na upako ulio juu yako na huduma yako. Ninatazamia kwa hamu kupokea na kusikia kutoka kwako.

Wako katika Kristo,

R.M. Port Harcourt, Nigeria

nao katika huduma. Mungu akubariki kwa wingi sana. Kwanza kabisa na kwa njia zote tuombee. Maombi huusukuma mkono wa Mungu. Bila maombi, huwa tunazunguka tu kama gurudumu. Tafadhalii, waombee wanafunzi wanaojitolea na wanaosafiri mbali kwenda vijijini na mili-mani kwa ajili ya kazi ya Bwana. Waombee wapate ujasiri, imani na upendo; tena, na Roho Mtakatifu awaongoze. Pia waombee, Mungu awakumbuke na kuwabariki. Tunaomba Mungu awape maisha marefu, amani na fanaka tele katika maisha yenu. Ninayewapenda katika upendo wa Kristo,

A.S.

Accra, Ghana

Mpendwa Mchungaji Tony,

Nashukuru sana kwa kunitumia kitabu chako kiitwacho, *Masihi*, na vijarida kumi. Vitu hivi vimeniletea mwamko wa kiroho na hamasa ya kumfanyia Mungu kazi katika maisha yangu. Niliwagawia wenzangu ambao walikuwa wamefisia katika imani. Wakati nilipowatembelea, walionesha furaha zao kwa kuwa walikuwa wamehuishwa kiroho na wanaendelea vyema baada ya kuvisoma vijarida hivyo. Watuhawa wana njaa ya majarida, kwa hiyo nakuomba unitumie vijarida 150 na Biblia kwa waumini wapya ambao wanazihitaji sana. Ninashukuru sana kwa maana naamini utanitumia. Asante kwa mafundisho yaliyo na utajiri mkuu wa Neno la Mungu ambalo umekuwa ukilitoa kwa uaminifu mkubwa. Mungu azidi kukubariki. Imani huhamisha mlima.

Binti yako katika Kristo,

T.O. Kumasi, Ghana

Mchungaji Mpenda,

Pokea salamu zangu kutoka huku Ghana. Baada ya kusoma makala yako iitwayo, *Masihi*,

Togo

Mpendwa katika Kristo,

Tuna furaha tele kupata barua yako. Pia tuna furaha kupokea machapisho mliyotutumia. Kwa hakika, Mungu anajidhihirisha kupitia kwayo. Tumefikia watu 15 ambao walijitoa kwa Kristo kupitia vijitabu vyako. Tunaomba kwamba Mungu azidi kuwabariki.

Tungependa kupata CD na Biblia za waumini wapya. Hali ilivyo sasa, hatutawenza kugharamia ununuvi wa vitu hivyo kwani Togo ni nchi masikini sana.

Tunatazamia kupokea CD hizo na Biblia ili kuzitumia katika mktarano wetu wa injili wa msimu huu wa Pasaka.

Baki na Baraka tele katika jina la Mtumishi

Rev. Henry James Lome, Togo

nina furaha tele kukujulisha kwamba mwishowe nimempokea Yesu Kristo kama mwokozi wangu; na kwamba alikuja na kufa kwa ajili yangu. Zamanii, nilikuwa duniani na sikumjua Mungu, wala sikumjua *Masihi*, Mwana wake. Lakini baada ya kusoma kitabu chako, sasa najua kuwa nilikuwa nimepotea na sasa nimepatikana, nilikuwa gizani, lakini Bwana Mungu amenileta nuruni. Kwa hiyo, mimi ni Mkristo ambaye nimezaliwa mara ya pili na Mwana wa Mungu. Kwa sasa sina Biblia na naomba ikiwezekana unitumie Biblia moja na kitabu chako kiitwacho *Masihi*. Ikiwezekana nitumie vitabu vingine vitakavyoweza kunisaidia kumjua Mungu zaidi, nitashukuru. Kwa sasa mimi ni mshiriki wa kanisa la Pentekoste huku Koforidua. Mungu akubariki kwa kazi nzuri ambayo umekuwa ukiitenda.

Wako Mwaminifu,

D.F. Koforidua, Ghana

USHUHUDA WA TONY ALAMO

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)

kwa miaka minge. Kila siku ninazidi kufahamu kwamba "sisi ni zaidi ya washindi" katika Kristo Yesu,²⁸ na "tumekamilika ndani yake."²⁹ Na pia ninafahamu jinsi ilivyo muhimu sana kufuata kila Neno la Yesu; ambaye alisema, wakati mfupi kabla tu ya kupaa kwenda Mbinguni mawinguni, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe."³⁰ (Hubiri kwa kila mfupa mkavu, yaani wale amba ni wafu kiroho ili wapate kusikia "Neno la Bwana"³¹)

"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."³²

Iwapo wewe ni kama mimi na hungetaka kuangamizwa bali uokolewe, omnia sala hii kwa Mungu:

BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi³³ ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.³⁴ Ninaamini kwamba aliku-fa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.³⁵ Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kuitia nguvu za ROHO MTAKATIFU³⁶ na

ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikili-za maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.³⁷ Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.³⁸ Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyoimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,³⁹ hutani-kataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yan-gu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.⁴⁰ NENO LAKO linasema hutamkataa ye-yote na mimi nikiwemo.⁴¹ Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.⁴² Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.⁴³

Baada ya kuokoka YESU alisema ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU.⁴⁴ Kwa makini soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938 na ufanye inavyosema.⁴⁵

BWANA anakutaka uwaambie wengine kuhusu wokovu wako. Un-

aweza kusambaza makala ya Injili ya mchungaji Tony Alamo. Tutakutumia makala hizi bila malipo. Tupigie simu ama ututumie barua pepe kwa habari zaidi. Mshirikishe na mtu mwingine ujumbe huu.

Iwapo unataka dunia yote iokolewa, kama YESU anavyoamuru, basi usim-wibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, "Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mme-niibia zaka na dhabihu. Ninyi mme-laaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili ki-wemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookole-wa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawa-fungulia madirisha ya mbinguni, na ku-wamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi" (Malaki 3:8-12).

28 Rum. 8:37; 1 Yoh. 4:3-4 29 Kol. 2:10 30 Mk. 16:15; Lk. 14:23 31 2 Fal. 20:16; Isa. 1:10; Yer. 2:4; Eze. 37:4 32 Mk. 16:16; 2 Thes. 2:12 33 Zab. 51:5; Rum. 3:10-12, 23
34 Mat. 26:63-64; 27:54; Lk. 1:30-33; Yoh. 9:35-37; Rum. 1:3-4 35 Mdo. 4:12; 20:28; Rum. 3:25; 1 Yoh. 1:7; Ufu. 5:9 36 Zab. 16:9-10; Mat. 28:5-7; Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21; 10:17-18; 11:25; Mdo. 2:24, 3:15; Rum. 8:11; 1 Kor. 15:3-7 37 Lk. 22:69; Mdo. 2:25-36; Ebr. 10:12-13 38 1 Kor. 3:16; Ufu. 3:20 39 Efe. 2:13-22; Ebr. 9:22; 13:12, 20-21; 1 Yoh. 1:7; Ufu. 1:5, 7:14 40 Mat. 26:28; Mdo. 2:21; 4:12; Efe. 1:7; Kol. 1:14 41 Mat. 21:22; Yoh. 6:35, 37-40; Rum. 10:13 42 Ebr. 11:6 43 Yoh. 5:14, 8:11; Rum. 6:4; 1 Kor. 15:10; Ufu. 7:14; 22:14 44 Mat. 28:18-20; Yoh. 3:5; Mdo. 2:38; 19:3-5 45 Kumb. 4:29; 13:4; 26:16; Yos. 1:8; 22:5; 2 Tim. 2:15; 3:14-17; Yak. 1:22-25; Ufu. 3:18

Tafadhalii wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:

Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078

Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362

www.alamoministries.com • info@alamoministries.com

Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani amba wanataka kumtumikia BWANA kwa miyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.

Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.

Tafadhalii wasiliana nasi kuitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.

Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiitwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.

Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kuitia meli.

Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhalii tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)
USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

Kwa wale amba mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo mtachapisha tena, tafadhalii jumuisha haki hii na usajili: